



## SIKU YA UKIMWI DUINIANI MWAKA 2008

Leo hii, mwaka wa 2008, ni mara ya ishirini ya kukumbuka siku ya UKIMWI ulimwenguni. *Uongozi* ndiyo dhamira kuu, chini ya wito “*Zuia UKIMWI, Tunza Ahadi*” Hii ndiyo kampeni inayoendelea pote duniani mpaka mwaka wa 2010.

Kwa miaka ishirini tumeona mengi, ujio wa madawa ya kuongeza muda wa kuishi, ongezeko la fedha kwa ajili ya kuzuia na kutibu, ujuzi zaidi uliosaidia kuongeza ufahamu wetu, kupanua mawazo na kupunguza unyanyapaa. Maendeleo haya yanaweza kufanya wengine wafikirie kwamba UKIMWI kati ya changamoto nyeti sana Afrika, bado inahitaji kutathminiwa kwa kupewa kipaumbele. Kwa nini tutoe fursa maalum, mali na utaalum kwa tatizo ambalo ni moja tu kati ya matatizo mengi?

Takwimu za Umoja wa Mataifa za mwaka 2008 zinatuuachia nafasi kidogo ya kutokuwa na wasiwasi. UKIMWI unandelea kuwa sababu kubwa ya vifo barani Afrika ambamo ni makao ya watu milioni 22 wenye virusi vya UKIMWI yaani theluthi mbili ya milioni 33 ya wenye virusi hivyo ulimwenguni. Kwenye ulimwengu unaondelea japo kuna maendeleo kiasi ya dawa za kuongeza muda wa kuishi, ikiwa na maana kwamba watu wachache zaidi wanakufa, tiba hii inawafikia baadhi tu ambao ni chini ya theluthi moja ya wanaohitaji huduma hiyo. Namba ya watoto yatima imeongezeka sana na mahitaji yao yaliyo mengi sana hayajakidhiwa. Mamilioni ya wengi walio barani Afrika bado wanaishi katika umaskini, shida na ukosefu wa taaluma hali ambayo inawaweka kwenye hatari ya kuambukizwa na virusi vya UKIMWI. Mengi yanahitaji kufanywa ili kubadili mwelekeo wa huu mkasa ulioenea sana.

Uzoefu wa Mtandao wa Wajezuiti wa Kushughulikia Maswala ya UKIMWI (AJAN), unatafsiri takwimu hizi katika hali halisi ya maisha. Wajezuiti wanaoshughulikia maswala haya kwenye karibu ya mataifa 30 barani Afrika, kusini mwa jangwa la Sahara, wanafahamu kwamba tiba, lishe bora, uchungaji mwema na matunzo ni haba kwa wale wote wanaovihitaji.

Profesa mmoja, anayetoa kozi juu ya maswala ya UKIMWI kwa watawa na waseminaristi, aliandika: *“Ninapata hisia kwamba hili swala la UKIMWI linapewa umuhimu mdogo zaidi na zaidi kati ya wanafunzi na katika jamii. Ninakuwa kweli na wasiwasi. Sijui kama hizi ni hisia zangu tu au ndivyo ukweli wa mambo ulivyo”* Kuendana na uzoefu wa AJAN, huo ni ukweli. Kwenye nyumba za malezi za Wajezuiti, baadhi ya watu huuliza swali kama kweli UKIMWI bado unastahili kuendelea kupewa

nafasi ya mbele hivyo, kama vile kuwa na mtandao ambao unashughulikia mambo hayo tu, kwa sababu siyo tena tatizo la dharura.

Kuanzishwa kwa Mtandao huo wa Wajezuiti wa kushughulika Maswala ya UKIMWI (AJAN) mwaka 2002, Wakuu wetu wa Shirika wa Afrika na Madagaska (JESAM) waliona hali hii ya UKIMWI kikweli kama hali ya dharura na inayostahili kupewa kipaumbele kishirika. Wakiamini kwamba Wajezuiti wana mchango wao maalum wa kuchangia katika kupambana na baa hili la UKIMWI. Mtandao huu wa kushughulikia maswala haya (AJAN) ni jibu la kunyumbulika la hali ya juu na ni wajibu wa muda mrefu kama zilivyo kazi zetu kuu za kitume. Hata mabadiliko yakitokea na rasimali zikinyauka, msimamo wa Shirika la Yesu ni ule ule wa kupamabana na UKIMWI hadi hapo utakapokoma.

Kazi nyingi zinafanywa na Wajezuiti kote Afrika, Kwa msaada na uratibu wa AJAN, wanatoa mchango wa Uongozi kwenye jumuiya, shule na vyuo vikuu, parokiani na kwenye familia: huduma mbalimbali za kimwili na za kitume, elimu kwa yatima; uwakili ili ipatikane tiba kwa wote; elimu ya kimaadili kama msingi imara wa kuzuia UKIMWI; utafiti wa kijamii na wa kiutauhidi.

Ni muhimu sana kuzingatia elimu. Mwaka huu, Dira Mpya ya Utume wa Wajezuiti wa Afrika na Madagaska inasisitiza, *elimu bora katika ngazi zote (msingi, sekondari, vyuoni, taasisi za huhuma za jamii na za kiroho, na kwenye parokia zetu) ni muhimu sana katika kuleta Afrika maendeleo ya uhakika na ya kudumu, na ndiyo njia wazi ambayo kwayo Afrika itaweza kupambana na changamoto zake katika ulimwengu huu wa utandawazi*, mojawapo ikiwa ni hili baa la UKIMWI. Ikiwa mstari wa mbele katika kupambana na UKIMWI, AJAN inafuata nyayo za mmoja wa walezi wake, Mwenye heri Anuarite, aliyejitoa katika maisha yake ya kitawa kuelimisha wengine mpaka alipokufa shahidi miaka 44 iliyopita.

Tumeitwa sio kunukulu, sembuse kushindana, bali

- kujitoa kwa upendo kwa wenye shida zaidi na wale waliosahaulika.
- kukuza huduma, kwa waathiriwa wa UKIMWI barani Afrika, kwa wingi, ubora na kina.
- Kuelimisha kwa kila hali hivyo kwamba Afrika inajizatiti vyema zaidi katika kukabiliana na UKIMWI.
- Kudhaminisha uongozi wa dira, ubunifu na utendaji.
- Kuleta imani, uhai na tumaini.

Ni vyema kuhitimisha ujumbe huu kwa busara ya wahenga: “Zingatia kwa moyo maneno yangu, ... nawe utaishi. Jipatie hekima, jipatie ufahamu” *Methali 4: 4 -5*.

Fratern Masawe, S.J.  
JESAM Moderator

1 December 2008